ilisema Dk Shein

Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anakuwa pia

Majina zaidi Uk.9

RAIA MWEMA. UK 2.

# *Wafugaji wateswa na biashara*

Na Mwandishi Wetu

KUPANDA kwa bei ya chakula na uingizaji holela vifaranga kutoka nje ya nchi, kumesababisha wazalishaji na wafugaji wazawa wa kuku kuacha kufuga wakilalamika kupata hasara.

Aidha, wameiomba Serikali kuweka mazingira wezeshi kwa wauzaji kuku kutumia mfumo wa kuuza kwa kilo kama wafanyabiashara wa nyama ya ng'ombe, mbuzi, kondoo na samaki.

Hayo yalisemwa jana Dar es Salaam na wazalishaji na wafugaji wa kuku wakizungumza na wanahabari kuhusu changamoto wanazopitia.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafuga Kuku (TABROFA), Costa Mrema alisema biashara ya kuku ina faida kubwa, iwapo taratibu na sheria zitafuatwa.

Hivyo aliiomba Serikali kuzuia biashara ya vifaranga kutoka nje kwa kuwa vinachangia kushuka kwa bei ya kuku sokoni na kuwasababishia hasara.

Alisema kuongezeka uingiaji wa vifaranga hivyo, umeporomosha soko la kuku kutoka Sh 5,300 hadi Sh 5,500, hali inayoumiza wazalishaji na wafugaji wa ndani.

"Biashara ya kuku ina faida kubwa sana, imeajiri vijana wengi wa kitanzania, ila tunaomba Serikali idhibiti uingizaji kuku kutoka nje kwani unaharibu soko la ndani," alisema.

Alisema kwa sasa Tanzania ni kama shamba la bibi katika sekta ya kuku, ambapo kila mtu anaingiza vifaranga na asilimia kubwa havina ubora.

Mshauri wa sekta ya kuku, Thabit Batenga alisema biashara ya vifaranga inapitia wakati mgumu kutokana na kukosekana kwa ushindani halali.

"Tumeamua kukutana na wadau wa sekta hii, ili kujadiliana namna ya kukabiliana na changamoto hii ya kukosekana ushindani halali, ili tupeleke serikalini kwa hatua zaidi," alisema.

Mfugaji, Flora Kamote alisema uingizaji vifaranga na bei ya chakula kupanda, imesababisha yeye kuachana na ufugaji kwa muda kwa kuwa mtaji wake unakwisha.

"Mimi nafuga kuku kutoka kampuni ya Organia, nimelazimika kuacha biashara hii sasa, mfano Oktoba nilipata hasara baada ya kuuza kuku 2,000 Sh 5,000 kila mmoja, huku gharama ya kukuza kifaranga hadi unamuuza, ni Sh 6,300," alisema.

Kamote aliiomba Serikali kuangalia changamoto hiyo kwa jicho la huruma, kwa kuwa madhara yake ni vijana na wanawake hasa wajane kukosa kazi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Organia, Albert Momdjian alisema vifaranga

Inaendelea Uk. 4

# Chato yapata madume 50 kuboresha ufugaji

Na Yohana Shida, Geita

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imetoa madume 50 ya ng'ombe wa kisasa kwa wafugaji wilayani Chato katika Mkoa wa Geita ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya mifugo na kuboresha sekta ya mifugo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Mandia Kihiyo alitoa taarifa hiyo baada ya kuwapokea ng'ombe hao katika mnada wa kisasa wa Buzirayombo wilayani humo.

Kihiyo alisema kwa sasa halmashauri hiyo ina takribani ng'ombe 100,000 wa kienyeji na akasema madume hayo ya kisasa yatagawanywa bure kwa vikundi 50 vya wafugaji.




Alisema madume hayo yatawezesha upatikanaji wa malighafi bora ya mifugo katika mnada wa kisasa wa Buzirayombo na wafugaji watapata ng'ombe bora wanaokua kwa haraka.

Mbunge wa Jimbo la Chato, Dk Medard Kalemani alihimiza wafugaji waitumie fursa hiyo na wayatunze madume hayo ili wawe na ufugaji wenye tija.

Dk Kalemani pia aliomba wafugaji wasiuze ng'ombe hao badala yake wawe wanawapeleka kwenye majosho ili kuzuia magonjwa.

"Mwaka jana tulipewa majosho sita, tumejenga, tumeyafungua, na yameanza kufanya kazi na mwaka huu tumepewa tena majosho sita ya zaidi ya Sh milioni 134 na tayari tunaendelea kujenga," alisema. Mwakilishi wa Wizara ya Mifugo, Jose Mtandiki alisema dume moja lenye umri wa mwaka mmoja na miezi minane lina uzito wa kilo 350 na thamani ya Sh milioni 2.6.

"Hii ni dhahiri kwamba serikali ya Rais Samia imekusudia kubadilisha hii sera ya ufugaji ambapo tunataka tufuge mifugo yenye tija siyo ng'ombe ana miaka mitano, ana uzito wa kilo 150," alisema.

# Sekta ya Uvuvi na mikakati ya kukuza mazao ya bahari



MCHUUZI wa samaki akiwa amebeba samaki katika Soko la Kimataifa la samaki Feri, Dar es Salaam.

Na ASHURA ASSAD

Serikali ya awamu ya sita na utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2021/22 2025/26 ulioanza hivi karibuni wenye lengo la kuboresha sekta ya uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayeshughulikia Uvuvi Dk. Rashid Tamatamah, anasema mafanikio na mikakati ya kukuza mazao ya uvuvi nchini ndiyo kipaumbele cha wizara kwa sasa.

Mpango huo unaolenga kukidhi matarajio ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ukiwa na lengo la kuboresha hali ya maisha ya watanzania kupitia mazao ya uvuvi.

Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, inatekeleza ilani yake kwa vitendo, lengo ni kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya uvuvi ili kuweza kuwa na uhakika na usalama wa chakula na lishe.

"Kupitia utajiri mkubwa wa rasilimali maji tuliobarikiwa na Mungu rasilimali hizi zinatakiwa kulindwa, kutunzwa, kusimamiwa, kuendelezwa, kuhifadhiwa na kutumiwa kwa njia endelevu ili ziweze kuchangia kikamilifu katika kutoa ajira na kuchangia pato la taifa," anasema.

"Kupitia utajiri mkubwa wa rasilimali maji tuliobarikiwa na Mungu rasilimali hizi zinatakiwa kulindwa, kutunzwa, kusimamiwa, kuendelezwa, kuhifadhiwa na kutumiwa kwa njia endelevu ili ziweze kuchangia kikamilifu katika kutoa ajira na kuchangia pato la taifa.

Anasema uchumi wa buluu ambao unahusisha bahari ni mkombozi wa wananchi kama ikitumika vizuri bahari na mazingira yake ni chanzo kikubwa cha mapato nchini.

Dk. Tamatamah anaongeza kuwa ili kufanikisha azma hiyo, Wizara inayo dhamira ya kuwa na sekta ya uvuvi endelevu na wa kisasa kiuchumi, kijamii na mazingira kufikia mwaka 2025.

Serikali inadhamiria kufanya mambo mengi yakiwemo ya kuwezesha sekta binafsi kuanzisha na kukarabati viwanda vya mazao ya uvuvi, kuhifadhi na kulinda maeneo tengefu ya bahari na maji baridi na kulinda na kuhifadhi makazi ya viumbe muhimu na viumbe wa majini walio katika hatari ya kutoweka.

Kwa mujibu wa Dk. Tamatamah uwekezaji katika miundombinu ya uvuvi, vifaa na ufugaji wa kibiashara wa samaki, kumewezesha upatikanaji wa mitaji, utalaamu, ujuzi, maarifa na zana za kisasa za uvuvi kwa wavuvi wadogo na wanawake kupitia vikundi vya kijamii.

Anasema kufungamanisha utafiti, ugani, uvuvi na kilimo cha majini, kudhibiti ubora, usalama na viwango vya mazao ya samaki na uvuvi, kuboresha maabara za uhakiki wa ubora wa rasilimali za majini na maeneo ya gati za uvuvi, kuwezesha kuhamasisha utalii katika maeneo tengefu ya bahari.

Katibu Mkuu huyo anasema pamoja na sekta hiyo kuwa miongoni mwa sekta za kipaumbele katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2021/22 – 2025/26, mchango wake katika Pato la Taifa (GDP) bado uko chini unachangia asilimia 1.71katika pato la taifa.

Mkurugenzi wa Idara ya ukuzaji viumbe maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dk. Nazael Madalla, anasema mafanikio na mikakati ya kukuza mazao ya uvuvi nchini itakuza tasnia ya ukuzaji viumbe maji na kusaidia kuongezeka kwa pato katika sekta hiyo.

Pia, Dk. Madalla anasema ni wakati muhimu sasa kwa wananchi kuendelea na ufugaji samaki ukizingatia kwa sasa serikali imekuwa ikiendelea kuimarisha vituo vyake vya ukuzaji viumbe maji ili kuhakikisha upatikanaji wa wingi wa vifaranga vya samaki maeneo mbalimbali kwa kujenga vituo vipya.

Kuhusu mazingira bora ya uwekezaji, anabainisha kuwa idara yake inaendelea kuboresha mazingira bora zaidi ya uwekezaji ili wananchi watakaoingia katika tasnia ya ufugaji samaki waweze kufuga kibiashara.

Mkurugenzi Msaidizi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayesimamia uendelezaji wa rasilimali za uvuvi, Merisia Mparazo, anasema mikakati ya kuendeleza sekta hii ni mikubwa ili kuongeza uzalishaji wa samaki.

Mparazo anasema kutokana na ongezeko la samaki katika maji ya asili kumekuwa kukichangia kutoa ajira kwa wingi katika sekta hiyo hivyo kuna haja ya kuzidi kuendeleza vipaumbele vyenye viashiria vya kukuza zaidi sekta hiyo.

Anasema uwepo wa upatikanaji wa samaki wengi zaidi watakaouzwa ndani na nje ya nchi na kuhakikisha kunapatika ajira za kutosha kwa vijana.

**UMUHIMU WA SEKTA YA UVUVI**

Kwa mujibu wa Merisia, umuhimu wa sekta hiyo unajidhihirisha katika kuchangia uchumi wa Taifa, lishe bora na ajira kuanzia katika ngazi ya familia.

Anasema zaidi ya watu milioni nne wameendelea kunufaika na sekta ya uvuvi ikiwamo uchakataji wa samaki, utengenezaji wa zana na vyombo vya uvuvi, biashara ndogondogo na mama lishe.

Mkurugenzi huyo anasema, changamoto zinazowakabili wawekezaji katika sekta ya uvuvi ni pamoja na

**"Kupitia utajiri mkubwa wa rasilimali maji tuliobarikiwa na Mungu rasilimali hizi zinatakiwa kulindwa, kutunzwa, kusimamiwa, kuendelezwa, kuhifadhiwa na kutumiwa kwa njia endelevu...**

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayeshughulikia Uvuvi.

upungufu wa maofisa ugani wa uvuvi ukilinganisha na mahitaji, upatikanaji wa vifaranga bora vya samaki.

Anasema serikali itaendelea kupambana na changamoto ya uvuvi haramu ili kuhakikisha rasilimali za uvuvi zinaboreka na hivyo kuchangia katika uchumi wa nchi.

MCHANGO KATIKA VIWANDA

Pamoja na changamoto katika sekta hii, ni ukweli usiopingika kwamba unapozungumzia Tanzania ya viwanda, huwezi kuacha kuitaja sekta ya uvuvi kama moja ya mzalishaji mkubwa wa malighafi za viwanda hususan vile vya nyama na usindikaji kwa ujumla.

Pia, katika mwaka 2016/2017, jumla ya tani 39,691.5 za samaki na mazao ya uvuvi yenye thamani ya Sh526.99 bilioni yaliuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa jumla ya Sh 14.30 bilioni kama ushuru.

Anasema serikali imeimarisha udhibiti ubora na usalama wa mazao ya uvuvi ili kulinda soko la ndani na nje ya nchi kwa kutumia maabara ya taifa ya uvuvi ya Nyegezi mkoani Mwanza.

**MKAKATI DHIDI YA UVUVI HARAMU**

Anasema serikali imezindua mkakati unaolenga kutokomeza uvuvi haramu, kwa kuanzisha operesheni ya kutumia ndege maalumu itakayofanya doria katika eneo la bahari kuu ili kudhibiti eneo hilo.

"Changamoto ya uvuvi haramu ni kubwa, mtu anapiga bomu katika matumbawe anafanya uharibifu ambao kuyatengeneza tena yanachukua zaidi ya miaka 100, huku yeye akiharibu kwa dakika tano, " anaeleza.

Anasema kutokana na teknolojia hii ya kisasa ya kutumia ndege katika doria, itasaidia kudhibiti kabisa uvuvi haramu katika ukanda wa nchi za Kusini Magharibi.

Anabainisha kuwa lengo la kuchukua hatua hiyo ni kuwezesha samaki wengi kuzaliana ili lengo la serikali la kujenga viwanda vya kusindika mazao ikiwemo viwanda vya kusindika minofu ya samaki lifanikiwe

Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaamini kuwa mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la taifa unaweza kupanda zaidi ya asilimia tano, iwapo kutakuwa na usimamizi na uvunaji endelevu wa rasilimali za uvuvi katika vyanzo vya mazao ya maji.

**WADAU WA UVUVI**

Wadau wa uvuvi nchini wameipongeza serikali kwa kuongeza nguvu ukuzaji viumbe maji na kuwasaidia wavuvi kupata tija kupitia mazao ya uvuvi.

Hassan Juma ni mmoja wa wadau wakubwa wanaofuga samaki kwa njia ya vizimba anasema mikakati ya kukuza mazao ya uvuvi nchini,itawasaidia wanaotaka kufuga samaki kutumia wataalam ili waweze kufuga kwa tija na kupata matokeo mazuri.

"Tunafurahi kuona changamoto zilizokuwa zinatukabili sasa zitashughulikiwa na sekta husika baadhi ya vipengele vya sheria ya uvuvi vilikuwa vikitupa changamoto wavuvi ni pamoja na tozo nyingi ambazo ni mzigo kwetu" anasema.

Anasema serikali ya awamu ya sita imekuja na utaratibu mzuri wa kushirikisha wadau wa sekta ya uvuvi katika maandalizi ya mabadiliko katika sekta hiyo.

Naye Mosha Mushi, anasema ni wakati mzuri kwa wataalamu kuwa na muda wa kuwatembelea wafugaji na kuwahamasisha namna ya kufuga kisasa kwa kuwa baadhi ya watu hawajui namna ya kuwapata wataalamu hao wa elimu ya ufugaji samaki.

Akitaja mojawapo ya kero ambayo wamependekeza ifanyiwe kazi ni leseni ya uvuvi; "Ikatwe leseni moja tu ya uvuvi na itumike katika wilaya zote ambapo mvuvi huyo atakwenda kufanya biashara."

Anasema serikali inatakiwa kutoa ulinzi madhubuti wa rasilimali za uvuvi, kuongeza uzalishaji na kuwa na masoko ya uhakika sambamba na kudhibiti utoroshwaji na uingizaji holela wa mazao ya uvuvi nchini.

Mushi anasema mabadiliko na matumizi ya sayansi na teknolojia katika uvuvi na ukuzaji viumbe maji ni kwenda sambamba na mahitaji ya ufugaji samaki katika mabwawa uliojitokeza miongoni mwa wananchi.

Anashauri kuwepo na udhibiti wa masoko na kuendeleza ukuzaji wa viumbe maji, kulinda mazingira katika maji na kukuza ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

Pia kuondoa vikwazo vya kibiashara na uwekezaji katika sekta ya uvuvi na kwenda na kasi ya mabadiliko ya serikali ya awamu ya sita ili kuikuza sekta hiyo.



MWANI uliomea vizuri baharini



Wanawake wakiwa wamebeba mabeseni ya samaki wa biashara